



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Nane – Tarehe 31 Mei, 2016.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2016/2017.

Mwenyekiti Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2016/2017.

II. MASWALI:

WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI, NA MICHEZO:

79. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (JIMBO LA CHAKE CHAKE) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiunga mkono Tamasha la Nchi za Jahazi (ZIFF), linalofanyika katika viwanja vya Ngome Kongwe ambapo sehemu kubwa ya tamasha hilo huchukuliwa na wasanii wa Kizazi kipya na kuziacha kabisa Ngoma za asili na michezo mengine ya kienyeji, ikiwemo mchezo wa ng'ombe hatimae kupelekea kutotambulikana katika ramani ya utamaduni wa hapa Zanzibar.

- a) Kuna utaratibu gani wa upangaji wa washiriki pamoja na sanaa zinazohitajika kuonyeshwa katika tamasha hilo la ZIFF.
- b) Serikali ina mpango gani wa kizifufua ngoma na Michezo ya asili ikiwemo mchezo wa ng'ombe ili irudi hadhi na haiba yake kama pale zamani.

WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:

42. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (JIMBO LA PAJE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Wananchi wa Makunduchi Tangi la Maji kwa muda mrefu wamekuwa wakipata umeme unaowaka chini ya kiwango (Low Voltage) na kuwapa wananchi wakati mgumu wakati wanalipia kama wananchi wengine wakati Shirika linalifahamu tatizo hilo lakini hakuna hatua zilizochukuliwa hadi leo hii.

- a) Je, lini Shirika litaondoa tatizo hili kwa wananchi hao ili nao wapate huduma hiyo kama sehemu nyengine.
- b) Je, Shirika limewafidia vipi wananchi walioathirika na tatizo hilo kutokana na umeme wanaoupata kuwa hauna uwezo wa kutumika katika shughuli za uwezeshaji au uhifadhi.

WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:

57. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (JIMBO LA CHUKWANI) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Wananchi wa Buyu walipewa ahadi na Rais wa awamu ya sita ya kutengenezwa barabara ya Chukwani Buyu. Na kwa kuwa Waziri dhamana wa wakati huo aliahidi mbele ya Rais na wananchi wa Buyu kuwa barabara hiyo ingetengenezwa ndani ya wiki mbili lakini ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa. Na kwa kuwa matengenezo ya barabara ya Shakani ambayo inaleta shida kwa wananchi wanaotokea Chukwani Buyu kuelekea Shakani mzunguko unakuwa mkubwa.

- a) Je ile ahadi ya Serikali ya kutengeneza barabara ya Chukwani Buyu kwa muda wa wiki mbili, itatekelezwa lini, wakati wiki mbili zimeshamalizika na sasa ni miaka mingi.
- b) Je kuna mpango gani madhubuti wa kutengenezwa barabara ya Shakani kupitia Kisauni ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Shakani.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2016/2017.

Zanzibar,
31 Mei, 2016.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA